# Barazani

Jarida la **Baraza la Habari Tanzania**
Toleo la **185, Oktoba, 2023**
ISSN **0856-874X**

*Kukuza Uhuru wa Vyombo vya Habari na kuhakikisha viwango vya juu kabisa vya weledi na uwajibikaji*



# Nimekamilisha - Mukajanga




**Mlay achaguliwa tena Rais MCT** Uk 5

**Mshindi wa EJAT ang'ara kimataifa** Uk 11

**Tido atunukiwa LAJA** Uk 15



Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa MCT wakipiga kura kumchagua Rais na wajumbe wa Bodi ya Baraza .

**MCT, MSHINDI WA TUZO YA IPI 2003 FREE MEDIA PIONEER**



**BODI YA UHARIRI:**
Kajubi Mukajanga Katibu Mtendaji – MCT
Hamis Mzee Mhariri

**MAWASILIANO**
Kwa Maoni na Malalamiko:
Katibu Mtendaji
Baraza la Habari Tanzani (MCT)
S.L.P. 10160, Dar es Salaam
Simu: +255 22 27775728, 22 2771947
Simu ya Kiganjani: +255 784 314880
Fax: + +255 22 2700370
Baruapepe: media@mct.or.tz
Tovuti: www.mct.or.tz
Facebook:- www.facebook.com/mediacounciltanzania Twiter:- www.twitter.com/mctanzania

# Mwisho wa zama

Baada ya miaka 15, Baraza la Habari Tanzania linapata uongozi mpya. Katika kipindi hicho Baraza lililojijengea umaarufu kwa sera yake ya vyombo vya habari kujisimamia, limepata mafanikio makubwa.

Na mafanikio haya ambayo Baraza linajivunia hayakupatikana kwa urahisi, bali kwa mapambano magumu ya muda mrefu.

Baraza lililoanzishwa na wadau walipopinga jaribio la serikali kuanzisha Baraza lake kudhibiti vyombo vya habari katika miaka ya 90, limekuwa na kuimarika na hatimaye kuwa chombo madhubuti cha kuendeleza vyombo vya habari.

Kwa kuungwa mkono na wadau wa habari na asasi za kiraia zenye mwelekeo sawia, mchakato wa kufanyia marekebisho vifungu vibaya vya sheria za habari Bara na Visiwani umeanza kufuatia shinikizo la washirika wa vyombo vya habari.

Zaidi ya hapo, Baraza limejihusisha pia na mafunzo ya wanahabari na limechapisha machapisho mbalimbali na vitabu vya kufundishia kwa maeneo mbalimbali.

Vyuo kadhaa vya uandishi wa habari sasa vinatumia mtaala ulioandaliwa na Baraza ambao umeidhinishwa na chombo cha serikali kinachosimamia mafunzo, Baraza la Taifa na Mafunzo ya Ufundi (NACTVET).

Katika miaka hiyo Baraza limefanya uchunguzi dhidi ya matukio ya ukiukwaji uhuru wa habari.

Shauri mojawapo na la aina yake ambapo Baraza lililichunguza kutokana na maombi ya kampuni ya Mwananchi Communications inayochapisha magazeti ya Mwananchi na The Citizen baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ambapo kampuni hiyo ililitaka Baraza lichunguze madai ya serikali kwamba gazeti la Mwananchi halikufanya haki katika kuandika habari kwa upande wa serikali katika uchaguzi huo.

Baada ya uchunguzi wa kina , timu ya watu watatu iliyoundwa na Rais wa Baraza, ililisafisha gazeti hilo kutokana na madai hayo.

Maeneo mengine ambayo Baraza lilipata mafanikio ni kufungua mashauri mahakamani na ushindi mkubwa ulikuwa ni kupinga Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 katika Mahakama ya Afrika Mashariki. Mahakama hiyo katika maamuzi yake, iliamuru kurekebishwa vifungu kadhaa vya sheria hiyo kwa kuwa vilionekana kwenda kinyume cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kutokana na mafanikio yaliyopatikana kuonekana kuwa mengi, uongozi mpya utakuwa na jukumu kubwa la kuendeleza mafanikio na lengo lake kuu liwe kuendeleza utaratibu wa vyombo vya habari kujisimamia ambao unakabiliwa na changamoto nyingi.




*Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, akihutubia Mkutano Mkuu wa 25 wa Baraza hilo ambapo alieleza kuwa anastaafu Desemba,mwaka huu.*

# Nimekamilisha, asema Mukajanga

**Na Mwandishi wa Barazani**

Mkutano Mkuu wa 25 wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) uliofanyika mjini Arusha Septemba 28, 2023 ulikuwa wa aina yake.

Kama kawaida ya mikutano ya aina hiyo wajumbe walipewa taarifa ya utekelezaji wa Baraza kwa mwaka uliopita katika maeneo na shughuli mbalimbali.

Tofauti na mikutano mingine, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo Kajubi Mukajanga, baada ya kuwa madarakani kwa miaka 15 tangu 2008 alitangaza kustaafu.

Katika hotuba yake iliyobebwa na neno 'NIMEKAMILISHA' Mukajanga aliwaeleza wajumbe jinsi alivyokamilisha malengo aliyokuwa nayo tangu aliposhika wadhifa huo.

Aliwaambia wajumbe wa mkutano huo, kuwa huo ndiyo mkutano wake wa mwisho akiwa Katibu Mtendaji wa Baraza hilo.

Alisema anastaafu Desemba, mwaka huu.

Hotuba kamili ya Mukajanga kwa wajumbe wa mkutano wa Baraza ambapo akielezea changamoto na mafanikio ya malengo aliyojiwekea ni kama ifuatavyo:-

Katika Mkutano Mkuu wa 10 wa Wanachama wa Baraza la Habari (MCT) Tanzania, uliofanyika tarehe 30 Julai 2008, Rais wa Baraza la Habari Tanzania wa wakati huo Profesa Issa Shivji alinitambulisha kwa wajumbe kama Katibu Mtendaji mpya, na kuwa ningeshika nafasi hiyo ndani ya mwezi mmoja na nusu.

Utambulisho huu ulikuja baada ya mkutano kati yangu na viongozi watatu wa Bodi ya Baraza tarehe 15 ya mwezi huo wa Julai, katika ofisi za Kigoda cha Mwalimu Nyerere cha Umajumui wa Afrika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambapo nilikutana na Profesa Shivji akiwa na Hayati Profesa Haroub Othman aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bodi ya Fedha na Utawala, na Hayati Jaji Mark Bomani aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili.

Katika mkutano huo viongozi hao watatu walioamini katika vyombo huru vya habari na mfumo wa vyombo hivyo kujisimamia vyenyewe, walinieleza kuwa nilikuwa nimechaguliwa na bodi kuwa Katibu Mtendaji baada ya mchakato uliokuwa umechukua takriban miezi sita. Walinieleza matarajio ya Bodi na kutaka kujua utayari wangu.

Kwa kifupi, tulikubaliana. Ndipo nilipoanza kuweka vizuri mawazo ya kile nilichotaka kufanya ambacho kingekuwa tofauti baada ya kuchukua hatamu. Hivyo, nilipopewa nafasi ya kusalimia wajumbe, pamoja na mambo mengine, niliainisha mambo matano ambayo nilikuwa nikiona yalihitaji kufanyiwa kazi. Leo ninapowaaga wajumbe wa Mkutano Mkuu huu, ningependa niyarejee, na niongee kwa kifupi pia kuhusu mengine tuliyofanikisha katika kipindi hiki.

Mambo hayo matano yalikuwa,

*Endelea Ukurasa wa 4*

# Nimekamilisha, asema Mukajanga

*Inatoka Ukurasa wa 3*

kwanza, Kuiimarisha Sekretarieti na mifumo yake; Pili, kuiweka MCT katika nafasi ya kimkakati katika tasnia ya habari; Tatu, MCT na klabu za waandishi wa habari.

Jambo la nne lilikuwa suala muhimu la Uhuru wa Uhariri; na mwisho MCT kumiliki nyumbani kwake.

**Kuiimarisha sekretarieti na mifumo yake**

Nilipoingia, nilikuta Baraza limeandaa Mpango Mkakati wake wa kwanza, uliokusudia kulifanya litende kimkakati na kuwa na utaratibu wa kuripoti ambapo matokeo ya kazi zake yangeweza kupimwa. Lakini lilikuwa na sekretarieti ndogo, skeleton secretariat, ambayo niliona isingeweza kumudu kuendesha taasisi kisasa na kwa viwango ambavyo sio tu vingetosha kuwaridhisha wanachama wake na wadau, bali pia kufanya wahisani mbalimbali kuliamini Baraza kama taasisi mujarab.

Kwa hiyo, jambo la kwanza lilikuwa ni kutathmini mahitaji ya nguvu kazi, kisha kutafuta na kuajiri watu wenye uwezo wa taaluma mbalimbali zilizohitajika, ambao wangeweza kuliendesha Baraza kufikia malengo kwa viwango vya juu, na nashukuru tuliwapata.

Jambo jingine lilikuwa ni kujenga mifumo imara. Hapo nyuma, kwa kuwa shughuli za Baraza zilikuwa chache, uendeshaji wake haukuwa mgumu sana (complex) na mifumo yake ilikuwa katika ngazi ya msingi (rudimentary). Sasa, kufuatia mpango mkakati wa kwanza ulioambatana na raslimali fedha nyingi na programu zilizohitaji uratibu mkubwa, tuliwajibika kuunda mifumo maridhawa ya raslimali watu, manunuzi, fedha, utawala, na kadhalika. Tuliajiri wataalamu washauri toka Kampuni ya Kazi Services Ltd. kutusaidia katika kuandaa sera mbalimbali, kisha tukawa na mafunzo kwa menejimenti na wafanyakazi.

Tulianzisha mfumo wa menejimenti uliozingatia matokeo, na kila mfanyakazi alijua nini alitarajiwa kufanikisha. Utendaji kazi wa wafanyakazi binafsi ulipitiwa walau mara mbili kwa mwaka, na watu walihimizwa kujiendeleza.

**Kuiweka MCT katika nafasi ya kimkakati**

Baraza la Habari lilikuwa tayari likifanya kazi nzuri na iliyokubaliwa na wanachama na wadau. Tulichofanya sasa ilikuwa kuendeleza pale tulipolikuta. Tuliazimia kulifanya Baraza kuchukua nafasi tatu muhimu kwa mpigo: nafasi ya Uongozi, nafasi ya Utumishi, na kutenda kwa Mashirikiano (team player).

Katika la kwanza, tuliazimia kujiwekea viwango vya juu katika kila kitu kilichofanywa na MCT, kuwa wa kwanza kubaini mahitaji ya wanachama na kuyashughulikia, kufanya kazi kwa uhuru na haki, kushirikisha wadau, na kuajiri watu walio bora katika nyanja zao.

Tulianza utoaji wa machapisho ya kitaaluma yenye ubora wa hali ya juu, na tukaanzisha vituo vya uhifadhi nyaraka na machapisho katika ofisi zetu za Dar es Salaam na Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya wanahabari na wanazuoni wa

*Endelea Ukurasa wa 6*



*Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 25 wa Baraza la Habari Tanzania uliofanyika Arusha Tanzania wakiwa katika picha ya pamoja.*



*Rais wa Baraza la Habari Tanzania, Jaji mstaafu Juxon Mlay, akiongoza mkutano Mkuu wa 25 wa Baraza kwa njia ya mtandao.*

# Rais MCT achaguliwa tena

**Na Mwandishi wa Barazani**

Rais wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Mwenyekiti wa Bodi, jaji mstaafu Juxon Mlay amechaguliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Yussuf Khamis Yussuf – Makamu wa Rais wa Baraza naye alichaguliwa katika Mkutano Mkuu wa Baraza uliofanyika mjini Arusha Septemba 28, 2023.

Wajumbe wapya watatu walichaguliwa katika uchaguzi huo. Ni Ali Mwadini, Dk. Rose Reuben na Sofia Komba.

Wajumbe wengine wa Baraza - Tido Mhando, Joyce Bazira, Happiness Nkya na jaji mstaafu Robert Makaramba pia walichaguliwa.

Rais wa MCT Jaji Mlay ambao aliongoza Mkutano Mkuu kwa njia ya Mtandao kutokea Mumbai , India, alikoenda kwa matibabu aliwaambia wajumbe wa mkutano huo kuwa Bodi imemteua Ernest Samson Sungura kuwa Katibu Mtendaji mpya wa Baraza.

Rais huyo alimtangaza kiongozi huyo wa Baraza mara baada Katibu Mkuu aliyepo madarakani , Kajubi Mukajanga kutangaza kustaafu kwake Desemba, mwaka huu.

Mukajanga alitangaza kustaafu kwake katika hotuba yake ya mwisho kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu ambapo aliwaelezea mafanikio mbalimbali yaiyopatikana katika kipindi cha miaka 15 ya uongozi wake.

# Nimekamilisha, asema Mukajanga

*Inatoka Ukurasa wa 4*

uandishi wa habari, yaani resource centres.

Katika lile la Utumishi, tuliweka utaratibu wa kutoa huduma zetu kwa haraka, bila njoo-kesho njoo-kesho, na kwa ubora wa hali ya juu. Tulisikiliza mawazo ya wadau na kuanzisha utaratibu wa kutembelea wanachama na hata wasio wanachama kusikia mawazo yao na kujua mahitaji yao. Tumekuwa tukisisitiza kwamba Baraza ni Mtumishi.

Kuhusu Mashirikiano, tukaanzisha utaratibu wa kuratibu shughuli zetu na washirika ili kuepuka utapanyaji wa raslimali fedha kwa kufanya yale ambayo tayari yanafanywa na wengine, na tukahakikisha mashirikiano kila ilipowezekana. Ni kutokana na utaratibu huo kwamba wanachama wa Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa – Coalition on Right to Information (CoRI), ambao sasa unajumuisha taasisi 16 za kihabari, kisheria na utetezi wa haki za binadamu, umekubali MCT kuendelea kuwa mwenyekiti wake na sekretariet.

### Klabu za Waandishi

Wakati nachukua nafasi ya Katibu Mtendaji, mradi wa Klabu za Waandishi wa Habari, uliokuwa chini ya MCT, ulikuwa ukiingia katika Awamu ya Pii na ya mwisho. Awamu hii ilikuwa ya miaka mitatu, na ilitakiwa baada ya miaka mitatu MCT ikabidhi mradi kwa UTPC.

Katika awamu hii ya mradi kulikuwa kuna msisitizo mkubwa katika mafunzo kwa waandishi na utoaji vifaa kwa klabu. Ilichukuliwa kuwa baada ya ile miaka mitatu klabu zingekuwa zimeshakomaa kuweza kuendesha mambo yake zenyewe na kujisimamia kama asasi kamili. Lakini niliposoma andiko la mradi nilibaini upungufu mmoja: hakukuwa na mkakati wowote wa kuzisaidia Klabu kusimama kama taasisi kwa maana ya kuzijengea stadi za uongozi, taratibu na mifumo, wala hakukuwa na mkakati kama huo kwa UTPC, na hakukuwa na exit plan ambayo ingehakikisha UTPC yenyewe imejengewa sekretarieti inayojitosheleza kwa kanuni, mifumo na sera mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji aliyekuwapo alikuwa amefanya kazi nzuri sana kuifikisha UTPC pale ilipokuwa, lakini ukweli ni kwamba alikuwa akibeba mzigo huo peke yake, na kumkabidhi majukumu zaidi bila sekretarieti imara ingekuwa ni kupoteza bure muda na rasilimali ambazo Mradi wa Klabu ulikuwa umetumia.



*Jengo jipya la Baraza la Habari Tanzania ambalo ujenzi wake unaendelea jinsi litakavyokuwa ujenzi ukikamilika.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninayo faraja kubwa kutamka kuwa changamoto hiyo tuliweza kuishughulikia, na hivi sasa UTPC ni kati ya taasisi bora na zenye mashiko katika kusimamia masuala ya wanahari nchini, na tunaendelea kufanya nayo kazi kwa karibu, pamoja na klabu za waandishi mikoani kote.

### Uhuru wa Uhariri

Suala la uhuru wa uhariri ni jambo jingine ambalo katika maono yangu, lilikuwa na umuhimu wa kutazamwa na kuona jinsi gani linasukumwa mbele. Nilisema wakati ule, na ninasema sasa, kuwa mara nyingi tunapoongelea uhuru huu huwa tunafikiria uhuru wa wahariri kutoingiliwa na mamlaka za kiserikali. Lakini pamoja na ukweli huo, sio serikali tu inayoingilia uhuru wa uhariri. Vipi wahariri kutoingiliwa katika kazi zao na watoa matangazo ya biashara na makampuni makubwa? Vipi uhuru wao kuhusiana na wanasiasa? Vipi viongozi wa kijamii na kidini? Vipi uhuru wa kutolazimishwa na wamiliki wa vyombo vyao kutenda kinyume na maadili ya taaluma?

Kwa hiyo tuliona hili jambo lilihitaji kuangaliwa katika mapana yake. Kwa hiyo tuliunda jopo la wajuzi (Think Tank), lililoongozwa na Rais Mstaafu wa MCT Profesa Issa Shivji, na kushirikisha wajuzi toka Tanzania, Kenya, Uganda na Marekani, kulitazama jambo hili kwa kina na mapana. Matunda ya kazi ya jopo hili ni Azimio la Dar es Salaam juu ya Uhuru wa Uhariri na Uwajibikaji, au The Dar es Salaam Declaration on Editorial Freedom, Independence, and Responsibility (DEFIR).

Hivi sasa DEFIR limesambazwa kote nchini na watu takriban 8,500 wametia saini zao wakiahidi kulifuata, kulitangaza na kulitetea azimio hilo. Pia limeingizwa, au liko katika mchakato wa kuingizwa, katika mtaala wa uandishi wa habari wa vyuo vikuu saba nchini.

Mkatati mwingine katika kukuza uhuru wa uhariri ulikuwa

*Endelea Ukurasa wa 8*



*Washindi wanne wa juu wa Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari waliowania ushindi wa jumla wa tuzo hizo wakiwa na mgeni rasmi, Katibu Mkuu Kiongozi Ombeni Sefue (katikati).*

# Washindi wa EJAT hawa hapa

**Na Mwandishi wa Barazani**

Wanahabari 60 wameibuka washindi katika kategoria mbalimbali za Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022.

Kati ya washindi hao 37 ni wanaume na 23 wanawake.

Katika tuzo hizo jumla ya wanahabari 92 kati ya 728 waliowasilisha kazi zao kuwaniaTuzo za Umahiri katika Uandishi wa Habari Tanzania(EJAT) 2022, waliteuliwa.

Kati yao 36 ni waandishi wa magazeti, 27 wa mitandao ya kijamii, 15 wa radio na 14 wa runinga.

45 kati ya wanahabari hao walioteuliwa ni wanawake ambapo 17 kati yao wanaandikia magazeti, 12 mitandao ya kijamii, sita redio na runinga 10.

Wanaume ni 47 ambapo kati yao 20 ni waandishi wa magazeti, 10 redio saba runinga na 10 mitandao ya kijamii.

Sanula Athanas wa gazeti la Nipashe aliibuka mshindi wa jumla.

Katika hatua hiyo ya kuwania kinyang'anyiro cha ushindi wa jumla, aliwatangulia wana fainali wenzie Francis Dhamira Kajubi wa The Guardian, Juma Mussa Issihaka wa Mwananchi na Anna Mbuthu wa TBC1.

Kwa ushindi huo, Athanas alikabidhiwa na mgeni rasmi Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu , Ombeni Sifue, tuzo, cheti na hundi ya mfano ya shilingi milioni tatu, fedha ambazo hutolewa na mshirika kiongozi wa EJAT, Baraza la Habari Tanzania (MCT) kumwezesha mshindi wa jumla kujiendeleza kwa mafunzo.

Washindi wa kategoria mbalimbali walipatiwa tuzo, vyeti na zawadi.

Orodha kamili ya washindi wa EJAT ni kama ifuatavyo:- Kategoria ya Wazi kwa mitandao ya kijamii Alfred Lasteck Mushi (BBC Swahili) Juma Mussa Issihaka (Mwananchi) – magazeti ambapo kategoria ya wenye ulemavu Mariam Shaban Mbwana (Mwananchi)–magazeti .

Heneliko Leonard Malo (Bomba FM) alishinda tuzo ya kuripoti jinsia na watoto – Redio, Kelvin Paul Matandiko (Mwananchi), Abel Claud Kilumbu (Dar24), Mwajuma Hassan Rajab (EATV) kwa runinga .

Jackline Victor Kuwanda (The Chanzo) aliibuka mshindi katika kategoria ya Mafuta, Gesi na Madini kwa mtandaoni

Ephrahim Edward Bahemu (Mwananchi), Herieth Isaya Makwetta na Baraka Mnyalei Loshilaa wote wa Mwananchi wallibuka washindi katika kuripoti Afya ambapo D'jaro Deus Arungu (TBC FM) alishinda kwa – Radio na Anna Thadei Augustino (EATV) mtandaoni.

Francis Dhamira Kajubi (The Guardian) alishinda katika kategoria ya Mazingira na Uhifadhi vyanzo vya maji kwa magazeti , Stanslaus Bernard Lambart (Dar24) mtandaoni , Anna Peter Mbuthu (TBC1) kwa runinga.

Kategoria ya Kilimo na Biashara ya Kilimo - Daniel Hezron Limbe (Malundeblog)– Mtandaoni, Anna Peter Mbuthu (TBC1) – runinga, Ayoub Stanley Nyondo (Shamba FM) –Radio .

Tuzo za kuripoti Haki za Binadamu kwa redio mshindi ni Said Ally Sindo (Storm FM), Janeth

Endelea Ukurasa wa 10



Baadhi ya wageni waalikwa wakiwa katika hafla ya kuwatunuku washindi wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022 katika ukumbi wa Mlimani City Jijini Dar es Salaam.

# Nimekamilisha, asema Mukajanga

*Inatoka Ukurasa wa 6*

kuwasaidia wahariri kuanzisha chombo chao imara.

Mbali ya kuilea UTPC katika siku za mwanzo ikiwa mradi, tulisimamia na kuwezesha uanzishwaji wa Jukwaa la Wahariri (TEF) na kulipatia bega la kuegemea kwa miaka mitano ya mwanzo, ikiwa ni pamoja na kuchangia kulipia gharama zake za uendeshaji na programu zake. Tuliamini katika lengo la TEF la kuunganisha wahariri kote nchini na kupigania uhuru wa uhariri.

**Maskani ya MCT**

Hii ilikuwa ni ndoto yangu nyingine niliyoongelea siku hiyo.

Harakati za kuifanikisha ndoto hii zimekuwa ndefu, na ngumu, kuliko nilivyotegemea siku hiyo nilipouahidi Mkutano Mkuu wa Kumi wa MCT kwamba Baraza lazima liwe na makazi yake lenyewe, liache kuendelea kuwa mpangaji.

Niliamini ningeweza kuwashawishi wahisani, na wanachama kuchangia jambo hili jema. Lakini pamoja na kwamba kila mmoja alikiri uzuri wa wazo lenyewe, mwitikio haukuwa wa kuchangia fedha.

**Ni hadithi ndefu, ya kusimuliana siku nyingine.**

Lakini leo ninayo faraja kubwa kusema tarehe 1 Februari, 2021 Baraza la Habari Tanzania lilihamia rasmi katika makazi yake Tegeta, Barabara Kuu ya Bagamoyo. Na sasa tumeshaanza upanuzi wa ofisi, tukijenga jengo la ghorofa mbili.

**Kwa hiyo, ndugu zangu, NIMEKAMILISHA.**

Leo nawaaga nikiwa na furaha, lakini, kwa hakika, kila kilichofanikishwa na Baraza katika kipindi cha ukatibu wangu kilifanikishwa kwa pamoja. Wafanyakazi wa MCT wamekuwa ni timu ya kupigiwa mfano. Kila kazi ilikuwa yetu sote. Tulishikana mkono, tulihimizana, tulisaidiana, na pamoja tulifanikisha mambo mengi. Na Bodi zetu zilituunga mkono.

Katika kipindi hiki, tulianzisha Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) ambazo zimekuwa kati ya tuzo bora za waandishi Afrika, na tumefanikiwa kuziendesha kwa miaka 14 bila kukosa. Tumeanzisha tuzo ya juu kabisa: Tuzo ya Maisha ya Mafanikio (LAJA), na tayari tumeshawatunukia wakongwe wetu saba.

MCT tumekuwa mshirika wa nguvu katika majukwaa ya mabaraza ya habari, hata nikachaguliwa kuwa makamu wa Raisi wa Umoja wa Mabaraza ya Habari Duniani (WAPC), na kisha Raisi wake, na sasa ni mwenyekiti mwanzilishi wa Umoja wa Mabaraza ya Habari Afrika Mashariki (EAPC).

Pamoja na uhaba wa raslimali fedha, kwa pamoja tumeweza kuiheshimisha Tanzania, kwa kuiwezesha MCT kuwa Baraza linalopigiwa mfano kote kote kama mfano wa self-regulatory system iliyofanikiwa zaidi.

Tumetoa majarida, vitabu, na miongozo ya uandishi habari ambayo inatumika katika vyuo vyetu.

Tumeweza kuandaa mitaala ya kufundishia uandishi ambayo imepitishwa na NACTVET na kufanywa mitaala ya kitaifa, na vyuo 21 vinatumia mitaala hiyo kufundishia.

Tumepeleka falsafa ya self-regulation katika vyumba vya habari kwa vitendo, kwa kusaidia vyombo vingi kuandaa sera zake za uhariri, stylebooks na internal codes of conduct.

Tumepeleka mapambano ya uhuru wa habari mahakamani, na kuyasaidia magazeti kadhaa kushinda kesi zake, wanahabari waliohukumiwa miaka 30 jela kuachiwa, na kupata ushindi mkubwa katika Mahakama ya Afrika Mashariki.

Kwa muda wote tangu Baraza lianze shughuli zake, mahesabu yamekaguliwa kila mwaka, na kwa wakati, na daima tumepata hati safi.

Katika kipindi hiki, uanachama wa MCT umezidi kuongezeka, kutoka taasisi wanachama 89 tulipoanza pamoja hadi 243 hivi sasa.

Tumeongeza majukumu na kupandisha hadhi ya ofisi ya Zanzibar, na Afisa Mdhamini wetu

*Endelea Ukurasa wa 23*



Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania, Kajubi Mukajanga, akizungumza katika siku ya Kimataifa ya Kupata Taarifa inayojulikana pia kama Siku ya Kujua. Kushoto ni Ofisa Mdhamini wa Baraza hilo ofisi ya Zanzibar Shiffaa Said Hassan.

# Mijadala yenye tija iruhusiwe - MCT

**Na Mwandishi wa Barazani**

Serikali imetakiwa kuruhusu mijadala yenye tija na afya kwa taifa badala ya kuizuia na kuwachukulia hatua watu wanaoianzisha.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupata Taarifa Septemba 28 ambayo pia hujulikana kama Siku ya Kujua Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari (MCT),Kajubi Mukajanga amesema kumekuwa na matukio machache yariyoripotiwa ya ubinyaji wa habari kwa waandishi kunyimwa habari, kutishiwa kukamatwa na ikiwamo kuzuiwa kwa mijadala ilihyohusu DP World.

Pia amewataka wananchi na waandishi wa habari, kutumia mitandao ya kijamii kwa umakini mkubwa katika kutoa taarifa sahihi na za ukweli ili kuelimisha umma.

Kimataifa kauli mbiu ya siku hii kwa mwaka huu ni Umuhimu wa Mitandao katika upatikanaji taarifa.

Baraza pia limetahadharisha kuhusu matumizi ya akili bandia ingawa ni kitu kizuri lakini kina changamoto zake.

Mukajanga katika taarifa yake amesema kuna baadhi ya watu waovu wanatumia teknolojia hiyo mpya ya akili bandia kupotosha umma, kuharibu sifa za baadhi ya watu ili kuwachafua na kuwaharibia shughuli wanazozifanya.

Ameutaka umma kuwa makini na taarifa za aina hiyo na kuepuka kuwa sehemu ya kutumia teknolojia hiyo kuharibu tswira ya nchi, jamii au mtu mmoja mmoja.

Mukajanga pia amehimiza serikali kuendeleza nia yake ya kuzifanyia marekebisho sheria zinazokwaza uhuru wa kujieleza, uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa waandishi wa habari na kuendelea kusikiliza maoni ya wadau na kuyafanyia kazi.

Alisema Baraza linegependa kuona serikali inazifanyia marekebisho sheria mbalimbali zikiwamo inayosimamia maudhui ya mtandaoni, sheria ya makosa ya mtandaoni, sheria ya kupata taarifa kuwezesha kupatikana taarifa kwa urahisi kwa wananchi.

Alieleza kuwa Baraza limeona marekebisho machache yaliyofanywa kwenye Sheria ya Huduma ya habari ya 2016.

Mukajanga pia alipongeza hatua zinazochukuliwa na Serkali ya Zanzibar kutunga sherioa mpya ya habari.

# Washindi wa EJAT hawa hapa

*Inatoka Ukurasa wa 7*

Kimaryo Joseph (Mwananchi) ,Asifiwe Brown Mbembela (The Chanzo) – mtandaoni, Omary Hussein Omary (Star TV) wa runinga.

Francis Dhamira Kajubi (The Guardian) na Cosmas C. Mwamposa (Pangani FM) waliibuka washindi wa kategeria ya kuripoti ushirika kwa magazeti na radio ambapo Khadija Ali Yusuph (Radio Jamii Mkoani) Pamela Nesphory Chilongola (Mwananchi), na Daniel Mwalubuli (NUKTA) waliibuka washindi katika kategoria ya kuripoti Biashara, Uchumi na Fedha.

Sanula Athanas (Nipashe) na Catherine M. Madabuke (Mazingira FM) waliibuka washindi katika kategoria ya kuripoti Utalii na Uhifadhi ambapo Hamis Makungu Hamisi wa Pangani FM, James Daudi Lerombo (TBC1), Juma Mussa Issihaka (Mwananchi) walibuka washindi katika Utawala Bora na Uwajibikaji.

Tuzo za Utamaduni, Sanaa na Michezo zilitwaliwa na Dauka Abraham Somba (Dar24), Clezencia Tryphone (Mwanasport).

Augusta Mathias Njonji (Nipashe), Adam Gabriel Hhando (CG FM), Heldina G. Mwingira (Dar24), Ahmadi Ally Mramba (TBC1) walitwaa Tuzo za kuripoti sensa ambapo , Grace Elibariki Mbise (Star TV) ,Sanula Athanas (Nipashe), Adam Gabriel Hhando (CG FM) , Suleiman Omary Mwiru, (NUKTA) walishinda tuzo za Kuripoti Elimu.

Elesia Thomas Haule (Azam TV) , Suleiman Omary Mwiru (NUKTA) na Warioba Igombe Warioba (Uhuru) walishinda Tuzo za Sayansi na Teknoloji.

Francis Dhamira Kajubi (The Guardian) na George Henry Helahela (Citizen Digital) walishinda uandishi wa Data, Juma Mussa Issihaka (Mwananchi) alishinda habari za uchunguzi , Najjat Haji Omar (The Chanzo) Uandishi wa habari za uchunguzi kwa mtandao.

Zuhura Juma Said (Zanzibar Leo), Dafrosa Prosper Ngailo (Azam TV) kategoria hiyo kwa TV, Festo Charles Lumwe (Dar24), na Peter Lugendo John (TBC Taifa) walishinda kategoria ya Jinsia na Afya ya Uzazi ambapo Baraka Mnyalei Loshilaa (Mwananchi) na Daniel Samson Mwalubuli (NUKTA) walishinda kategoria ya kodi na ukusanyaji mapato.

Festo Charles Lumwe (Dar24), Naishooki Alais Makeseni (Star TV) walishinda katika kategoria ya kuripoti wenye ulemavu ambapo , Hazla Omary Quire (TSN Digital) alishinda katika kategoria ya Utalii na Uhifadhi.

Jopo la majaji saba wanahabari mahiri wenye uzoefu mkubwa chini ya uongozi wa mhariri mkongwe Mkumbwa Ally walipitia kazi zilizowasilishwa kuwania tuzo hizo.

Mashirika na taasisi mbalimbali zilichangia EJAT kifedha ambayo ni Mamlaka ya Bandari (TPA), Tume ya Ushirika (TCDC), Marie Stopes Tanzania (MST), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Ushirikiano na Maendeleo la Uswisi (SDC), Shirika la Misaada la Kimataifa kwa Vyombo vya Habari (IMS), Mfuko wa Hifadhi wa Jamii (PSSSF) Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), Azam Media Group, Coca Cola Ltd, Busota Inn, WWF, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Mamlaka ya Maji Dar es Salaam (DAWASA) na UMATI,




*Mshindi wa Jumla wa Tuzo za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) Sanula Athanas wa gazeti la Nipashe akipokea hundi ya mfano ya sh. milioni tatu ikiwa sehemu za zawadi kwa ushindi huo.*




*D'jaro Arungu wa Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), akionyesha tuzo mbili za Shining Stars Africa Awards 2023 alizoshinda.*

# Mshindi wa EJAT ang'ara kimataifa

Na Mwandishi wa Barazani

Mshindi wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022 katika kundi la Afya, kipengele cha redio, D'jaro Arungu wa Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), ameshinda tuzo mbili za Shining Stars Africa Awards 2023.

Hafla ya utoaji tuzo hizo ilifanyika Septemba 2, 2023 kwenye ukumbi wa Cotton Lounge jijini Johannesburg, Afrika ya Kusini ambapo D'jaro ameshinda tuzo mbili ambazo ni Best Radio Personality of the Year Awards na Best Star Inspirational Man of the Year.

Kwa mujibu wa D'jaro, ushindi wa tuzo za EJAT umemtia nguvu na hamasa kubwa yeye kama mwandishi kwa kuwa ni tuzo zinazotolewa kwa kuzingatia weledi wa hali ya juu.

"EJAT ni tuzo zinazotolewa kwa kuzingatia weledi wa kitaaluma kwani kazi husika hupitiwa na majaji ambao mara zote huwa ni waandishi waliobobea kwenye taaluma", alisema D'jaro.

D'jaro aliongeza kuwa Shining Stars Africa Awards zenyewe huanza na kupendekezwa na wasikilizaji au washabiki wako, hivyo kuna wakati tunaweza sema kuwa hata wale wanaokupendekeza au kukupigia kura sio lazima wawe wanataaluma husika.

Awali D'jaro alisema kuwa kuna baadhi ya watu walikuwa wakimbeza kwa kuwa alikuwa anashinda tuzo za kupendekezwa na wasikilizaji, lakini kwa sasa amewadhihirishia Watanzania na wanataaluma wenzake kuwa yeye ni mwandishi bora ambae ameshindi tuzo za EJAT lakini pia zile za Shining Stars Africa Awards.

# Washindi wa EJAT 2022



*Washindi wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2022 wakiwa na mgeni rasmi Katibu Mkuu Kiongozi, Ombeni Sefue ( wa nne kutoka kushoto mstari wa mbele) na waheshimiwa wengine.*



*Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu,Balozi Ombeni Sefue , akizungumza katka kilele cha Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022.*

# Habari si lazima ziwe mbaya - Balozi Sefue

**Na Mwandishi wa Barazani**

Waandishi wa habari wameambiwa kuwa habari siyo lazima ziwe mbaya.

Akizungumza katika kilele cha Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania kwa mwaka 2022 zilizofanyika Julai 22, 2023 katika Ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Ombeni Sefue alisema si vema kuwaaminisha wananchi kuwa habari lazima ziwe mbaya, na kuwajengea kiu ya kashfa, matusi, uhalifu na uozo.

Aliwasishi wanahabari wasiendekeze msemo kwenye uandishi wa habari usemao habari, "ikiwa mbaya sana, lazima inavutia, na ikiwa sio mbaya sana, lazima inachosha".

Katiku Mkuu Kiongozi Sefue katika hotuba yake iliyopewa kichwa Elimika Uelimishe, alisema tatizo lingine linajitokeza katika uandishi wa habari linahusu kile kinachoandikwa.

"Sehemu kubwa ya yale yanayoandikwa hayajihusishi na masuala mazito ya maendeleo na utawala bora, ambayo ni muhimu kwa ustawi wa watu wetu walio wengi," alisema na kuongeza kuwa "na, mbaya zaidi, baadhi ya yale yanayoandikwa yanakiuka heshima ya Kiafrika, heshima kwa mamlaka, na haki ya watu wanaochafuliwa kujibu na kujisafisha mbele ya jamii".

Pia alisema wakati mwingine, kile kilichoandikwa ni cha kiwango cha chini, kisicho cha kitaalamu na kisicho na maadili, akasisitiza kuwa hataki kuamini kuwa hilo ndilo lengo la kudai uhuru wa vyombo vya habari.

Balozi Sefue akizungumzia uhusiano mzuri kati ya serikali na vyombo vya habari, alisema kunahitajika kuaminiana ambako kutaletwa na mambo mawili ya msingi.

Alisema kwanza, vyombo vya habari na waandishi wa habari lazima wawe na weledi wa hali ya juu na wawe waadilifu.

Pili, alisema, wanasiasa na watawala lazima wabadili fikra kutoka kuviona vyombo vya habari kama wasumbufu tu, isipokuwa pale vinapowasifu.

Alisema wanahabari "wakikosoa, wanageuka wasumbufu. Hii si sahihi, ili mradi ukosoaji uwe umetokana na utafiti wa kina ili kuelewa jambo lenyewe na mazingira yake kabla ya kukimbilia kuhukumu na kukosoa".

Kwa waandishi, alisema, wasikimbilie kukosoa kabla ya utafiti na kuelewa jambo lenyewe vizuri na mazingira yake,na ndipo watakuwa na haki ya kudai Serikali iwe wazi kwao na kuongeza "hapo mtakuwa na haki ya kukosoa panapostahili kukosolewa".

Alisema Serikali na vyombo vya habari vilivyo makini ni miguu miwili ya mfumo wa utawala bora wa kidemokrasia.

Balozi Sefue alisistiza umuhimu wa pande hizo mbili kukubali na kujifunza kila siku kuishi kwa kushirikiana na kuvumiliana kuzingatia utashi wa maslahi ya umma.

"Utawala bora ni utawala shirikishi, si kupitia tu kwa wabunge na madiwani, bali pia kwa kutoa fursa ya kusikia hoja na maoni ya wananchi wa kawaida, na vyombo vya habari ni njia mojawapo ya kufanya hivyo", alisema.

Waandishi wa habari walio makini, alisema, wanayo nafasi nzuri ya kuelimisha wananchi kuhusu mambo mbalimbali ili wananchi hao wawe na msingi wa kushiriki vema mijadala ya mwelekeo wa taifa.

Utawala bora unalenga kufikia mwafaka katika jamii na taifa, ikiwemo mwafaka wa mwelekeo, mwafaka wa sera, mwafaka wa utendaji na mwafaka wa tathmini.

Aidha alisema, unatafuta kupatanisha fikra mchanganyiko, na maslahi yanayokinzana katika jamii.

Balozi Sefue alipongeza MCT kwa uamuzi wa busara wa kuanzisha tuzo za EJAT, na kuzidumisha kwa miaka yote hii, licha ya changamoto mbalimbali.

"Kwa kufanya hivyo mmefanikiwa kuendeleza utamaduni huu wa kujitathmini na kuwatambua na kuwazawadia waandishi bora wa habari," alisema na kuongeza, "mmefanya kuwepo na sababu ya waandishi wa habari kufanya lililo zaidi, na kuibua vipawa vyao, ili wawe bora zaidi na hili ndilo wananchi wanalolihitaji, na bila shaka Serikali vilevile".

Aliwasihi waandishi wa habari wengi iwezekanavyo kushiriki tuzo za EJAT ili kujitathmini na kujipa motisha ya kufanya vizuri zaidi.

Pia aliitaka Serikali itambue kuwa, kwa kuhamasisha uboreshaji wa taaluma ya uandishi wa habari, tuzo za EJAT ni mdau muhimu katika

# Tido atunukiwa LAJA

## ● Awaasa wanahabari walinde hadhi, heshima zao

Na Mwandishi wa Barazani

Waandishi wa habari nchini wameaswa walinde hadhi na heshima zao kwa kutokubali mlungula, mishiko maarufu kama brown envelope.

Maneno haya yamo katika ujumbe mahsusi wa mtangazaji na mwandishi nguli, Tido Dunstan Mhando, aliotuma akiwa London, Uingereza katika kilele cha Tuzo za EJAT kilichofanyika katika ukumbi wa Mlimani City Dar es Salaam Julai 22, mwaka huu.

Katika shehere ya tuzo hizo ambapo Baraza la Habari Tanzania (MCT) na washirika wake huwatambua na kuwatunza wananahabari kwa kufanya kazi nzuri katika kipindi cha mwaka uliopita, Tido alitunukiwa Tuzo ya Mafanikio ya Maisha katika Uandishi wa Habari (LAJA) kutokana na mchango wake mkubwa uliotukuka katika kuendeleza taaluma na uhuru wa habari.

Tido alikuwa London kwa matibabu na Tuzo yake ilipokelewa kwa niaba yake na baba yake mzazi Mchungaji Daniel S. Mhando (99).

Katika ujumbe wake alioutoa akiwa London ambao ulionyeshwa katika kilele cha EJAT, Tido alisema kwa maisha yake ya miaka 55 katika uandishi wa habari ambayo yamekuwa ya kupanda na kushuka anashukuru MCT na washirika wake kwa kumpatia tuzo hiyo ambayo ni zawadi kubwa na adhimu kwake.

"Nina furaha kubwa … na tuzo hii nimepewa wakati muafaka kwani sasa ni wakati wa kuachia ngazi", alisema nguli huyo wa utangazaji na uandishi aliyeanzia kufanya kazi katika iliyokuwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), ripota wa mashirika mbalimbali na Shirika la Utangazaji wa Uingereza (BBC) alipopanda na kuwa mwafrika wa kwanza kuwa mkuu wa Idhaa ya shirika hilo.

Hivi sasa Tido ni Mtendaji Mkuu wa Azam Media yenye Azam TV and U FM Radio.



Mwanahabari nguli na Mkurugenzi Mkuu wa Azam Media, Tido Mhando akizungumza kutoka London Uingereza baada ya kupewa Tuzo ya Mafanikio ya Maisha katika Uandishi wa Habari (LAJA).

Alijiunga na RTD 13 Januari, 1969, akiwa na umri wa miaka 21.

Mwanzoni alijikita zaidi kwenye vipindi vya muziki na vijana. Kipindi cha muziki cha Dunia ya Jumamosi na cha vijana cha Salamu za Vijana vilipendwa sana.

Baadaye akaanza kutangaza mpira ambapo mwaka 1973 ndiyo ulikuwa mwanzo wa mabadiliko makubwa kwenye maisha yake ya utangazaji.

Uganda ya Iddi Amin walikuwa wenyeji wa mashindano maarufu ya soka siku hizo, Challenge Cup, ya Afrika Mashariki na Kati.

Akachaguliwa yeye na Mshindo Mkeyenge kuambatana na Taifa Stars kwenda Kampala. Hii ikawa safari yake ya kwanza nje ya nchi. Kutokana na hali ya mashaka baina ya Tanzania na Uganda ya Amin, sharti kubwa walilopewa lilikuwa kutotoka katika hoteli ya Emperio waliyofikia zaidi ya kwenda tu uwanjani Nakivubo na kurudi.

Mwaka 1979 alipoambatana na Taifa Stars kwenye mashindano mengine ya Challenge nchini Kenya ndipo alipokutana na Simon Ndesandjo aliyekuwa mmiliki wa kampuni ya kutengeneza vipindi vya radio vya kibashara ya High Fidelity Production Limited aliyemtaka kujiunga na kampuni yake.

Aliondoka RTD kimya kimya mapema mwaka 1980. Huu ukawa mwanzo wa safari yake ndefu ya kiasi cha miaka 30 ya kufanya kazi nchi za nje.

Alikaa High Fidelity kwa muda wa miaka minne akaamua kuacha na kuwa mtangazaji wa kujitegemea, akibadili mwelekeo na kuingia kwenye utangazaji wa habari na matukio. Anasema hajawahi kujutia uamuzi huo, kwani ulimfungulia ukurasa mpya katika maisha yake ya utangazaji.

Akafanikwa kupata kazi ya kuwa ripota wa Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Amerika, VOA, na muda mfupi baadae Idhaa ya Kiswahili ya BBC. Mara Sauti ya

Endelea Ukurasa wa 16




*Mchungaji Daniel S. Mhando (99) akipokea kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu , Ombeni Sefue, Tuzo ya Mafanikio ya Maisha ya Uandishi wa Habari (LAJA) kwa niaba ya mwanawe, Tido Dunstan Mhando. Kushoto ni mdogo wake Tido Prof. Martin Mhando na kulia ni watoto wawili wa Tido.*

# Tido atunukiwa LAJA

*Inatoka Ukurasa wa 15*

Ujerumani, DW nao wakamwomba kuwapelekea ripoti. Akawa mwakilishi wao, siyo Kenya pekee bali kwenye nchi zote za Afrika ya Mashariki na Kati ikiwa ni pamoja na Tanzania, Uganda, Ethiopia, Rwanda, Burundi, Sudan, Sudan Kusini, Somalia na Msumbiji.

Anakumbuka kuwa hiki kilikuwa kipindi cha heka heka nyingi katika eneo hilo ambalo yeye alikuwa mwakilishi.

Uganda kulikuwa na harakati za Yoweri Museveni, John Garang huko Sudan Kusini; Msumbiji nako vita baina ya Renamo na serikali ya Frelimo.

Nchini Tanzania kulitanda shauku ya mabadiliko ya uongozi baada ya Mwalimu Nyerere kuamua kung'atuka, wakati Kenya kwenyewe kulikuwa na mshike mshike wa kudai mabadilliko ya kisiasa ya kuleta vyama vingi.

Kuripoti kuuawa kwa Dk. Robert Ouko aliyekuwa waiziri wa mambo ya Nchi za Nje wa Kenya, kulimwongezea yeye sifa kama mwanahabari. Alikuwa wa kwanza kuripoti kupotea kwa waziri huyo ambaye hatimaye alipatikana akiwa ameuawa.

Dk. Ouko alikuwa Waziri chini ya Rais Daniel arap Moi na alikuwa maarufu mno miongoni mwa Wakenya, na siyo kwao tu Ujaluoni bali nchini kote. Alikuwa mzungumzaji mzuri mwenye wajihi wa kuvutia. Wengi wakimlinganisha na mwanasiasa mwingine mashuhuri wa zamani nchini humo, Tom Mboya, aliyeuwawa kwa kupigwa risasi hadharani mtaani Nairobi, Julai 1969.

Baada ya hapo Tido alihamia London kupata mafunzo na kufanyakazi BBC ambapo katika utumishi wale alipata fursa ya kuripoti masuala mbalimbali makubwa ya kisiasa ya kanda hii ya Afrika ikiwemo matukio ya Rwanda, Burundi na Congo DRC.

Alitumikia BBC kwa miaka 21 ambapo mwaka 1999 aliteuliwa kuwa mkuu wa Idhaa ya Kiswahili.

Katikati ya mwaka 2005 baada ya Rais Kikwete kuteuliwa kuwa mgombea wa urais kwa tiketi ya CCM, aliombwa na ubalozi wa Tanzania London aende uwanja wa ndege wa Heathrow kukutana naye uwanjani akiwa njiani kwenda New York, Marekani, kuhudhuria kikao cha Umoja wa Mataifa.

Kikwete alimwomba arudi nyumbani ili atakapokuwa Rais, yeye aziongoze taasisi za utangazaji za serikali, yaani RTD na TVT ambapo Tido alikubali bila kusita.

Aliwasili TVT na RTD akiwa na ari ya kufanya maboresho stahiki tena kwa haraka.

Kazi yake kubwa ya kwanza ilikuwa kuziunganisha taasisi hizo mbili kuwa moja. Mwezi Agosti 2008 TBC ikazaliwa rasmi katika sherehe ya uzinduzi iliyohudhuriwa na Rais Jakaya Kikwete.

Baada ya hapo ikawa kazi mtindo mmoja, lengo kuu likiwa kufanikisha nia ya shirika kupunguza utegemezi wa kifedha kwa serikali. Pia mageuzi kwenye maudhui, ili kuwafanya Watanzania kulipenda shirika lao la utangazaji.

Yakatangazwa mabadiliko ya kutoka kwenye mfumo wa analog kwenda kwenye digiti kwa usambazaji wa matangazo ya televisheni.

*Endelea Ukurasa wa 23*

# Umuhimu wa elimu ya jinsia katika vyombo vya habari nchini

Na Tumbi Kiganja

Tatizo la uwiano wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume limekuwa changamoto kwa miaka mingi katika jamii zetu za Kitanzania kutokana na kasumba inayotokana na sababu mbalimbali ikiwemo mfumo dume, mila na desturi.

Hali hii ya kutokuwa na uwiano baina ya wanaume na wanawake imekuwa ikileta changamoto na kuathiri maeneo mbalimbali ikiwemo siasa, uchumi, jamii na teknolojia pia.

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na jitihada mahsusi za kuhakikisha suala la usawa wa kijinsia linapewa uzito. Jitihada hizi zimekuwa zikihusisha vyombo vya habari ili kutoa elimu kwa umma.

Jitihada hizi zimekuwa zikifanywa na serikali pamoja na wadau mbalimbali ikiwemo Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Kwa miongo miwili sasa MCT imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa jinsi vyombo vya habari vinavyoripoti masuala mbalimbali ikiwemo jinsia.

Ripoti zimekuwa zikionyesha kuwa kumekuwa na mabadiliko ya namna vyombo vya habari vinavyolichukulia suala la jinsia kwa maana ya namna habari zinavyoripotiwa kwa kuzingatia usawa na aina ya vyanzo vya habari vinavyotumika.

Pia, ripoti zimezingatia namna gani waandishi wa kike na kiume wamekuwa wakipewa majukumu ya kila siku. Kwa mfano, aina zipi za habari au makala ambazo waandishi wa kike na kiume wamekuwa wakitumwa kuzitafuta au kuandika; kati ya habari zinazochapishwa kwenye kurasa muhimu, ngapi zimeandikwa na wanawake na ngapi wanaume.

Mwaka 2013 MCT ilichapisha mwongozo wa kufundishia masuala ya jinsia katika vyuo vya uandishi wa habari ambao ulifanyiwa mapitio na kuchapwa upya mwaka 2021 na kuzinduliwa Julai 12, 2022 na Rais wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jaji Juxon Mlay kwenye hoteli ya Seashells Millennium iliyopo Kijitonyama, Dar es Salaam.

Wakati wa uzinduzi wa mwongozo huo, Jaji Mlay alisema kuwa kitabu cha kufundishia masuala ya jinsia, kiwe chachu kwa wakufunzi wa uandishi wa habari pamoja na waandishi kwa kuchagiza uandishi wa habari wenye jicho la jinsia.

Tangu mwongozo huo uzinduliwe mwaka 2022, hadi sasa jumla ya wakufunzi 25 toka vyuo mbalimbali vinavyofundisha uandishi wa habari nchini wamepatiwa mafunzo na MCT kuhusu masuala ya jinsia na vyombo vya habari.

Wakati wa mafunzo hayo ambayo yalitolewa kwa nyakati mbili tofauti kwa njia ya mtandao, Desemba 02, 2022 na Septemba 6, 2023 Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania, Kajubi Mukajanga aliwasisitizia wakufunzi hao kuwajengea uelewa wanafunzi wao kuhusu masuala ya jinsia.

Mukajanga alisema kuwa "ipo haja ya kutengeneza taswira chanya ya wanawake katika vyombo vya habari, na ili kulifanikisha hili ni lazima wakufunzi wahakikishe wanatoa elimu ya kutosha ya masuala ya jinsia kwa wanafunzi ambao ndio waandishi wa habari wa siku zijazo"

Aidha, Mukajanga alisema kuwa hakuna taifa linaloweza kuendelea ikiwa litaiacha nyuma jinsi moja. Wanawake na wanaume ni jinsia zinazotegemeana hivyo kuiacha moja nyuma ni kukwamisha maendeleo ya jamii husika," aliongeza.

Kwa upande wake mwezeshaji wa mafunzo hayo ambaye pia ni mtaalamu elekezi wa masuala ya habari, Pili Mtambalike, alisema kuwa mwongozo huu ulioandaliwa na MCT ukitumika vizuri utasaidia kujenga waandishi imara ambao wataweza pia kutekeleza haki na usawa wa jinsia kwenye vyombo vyao.

"Wakufunzi wajipe muda wa kupitia na kuusoma mwongozo huo wa jinsia ambao una maudhui ambayo yatasaidia kujenga na kuandaa waandishi wenye uelewa na mazingatio kuhusu jinsia," alisema Mtambalike.

Wakitoa michango yao katika mafunzo hayo wakufunzi walisema kuwa mwongozo huo ni hazina kubwa kwa tasnia ya habari na taifa kwa ujumla na unapaswa kutumiwa katika vyuo vya uandishi na vyombo vya habari.

Suleiman Seif Omar kutoka Chuo Kikuu Zanzibar alisema kuwa bado kumekuwa na changamoto kubwa sana katika vyombo vingi vya habari kuhusu namna ya kuripoti habari zao kwa kuzingatia jinsia.

"Ni kawaida kwa baadhi ya jamii kutowaamini wanawake; jambo ili liaminike basi lazime kuwe na sauti ya mwanaume. Hii pia inafanya baadhi ya vyombo vya habari kuwa na mlengo wa namna huu. Kitu hiki ni hatari sana kwa tasnia ya habari nchini," alisisitiza Suleiman Seif Omar.

*Endelea Ukurasa wa 20*




*Rais wa Mahakama ya Afrika , Jaji Imani Aboud, akifungua mkutano wa kanda kuhusu usalama wa waandishi wa habari uliofanyika katika ukumbi wa mahakama hiyo, mjini Arusha. Kushoto ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari, Kajubi Mukajanga.*

# Mahakama ya Afrika kuendelea kulinda haki za wanahabari, kujieleza

Na Mwandishi wa Barazani

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu yenye makao yake mjini Arusha imeahidi kutumia kila fursa kuendeleza haki ya kujieleza na kulinda haki za waanadishi wa habari katika maamuzi yake ya kimahakama.

Akifungua mkutano wa Kanda kuhusu usalama wa waandishiwa habari, Rais wa mahakama hiyo, Jaji Imani Aboud, alisistiza kuwa kudumisha kwa uhuru wa kujieleza sambamba na haki za waandishi wa habari ni suala la wadau wote.

Aliwaambia wajumbe wa mkutano huo uliofanyika Septemba 29 katika ukumbi wa Kibo katika makao makuu ya mahakama hiyo kuwa Umoja wa wa Mataifa unatambua kwamba uandishi wa habari ni kazi ya hatari.

Alisema umoja huo unasema kuwa ingawa uandishi wa habari ni muhimu kwa maendeleo endelevu, haki za binadamu na kuimarisha demokrasi, ni kazi hatari akiongeza kuwa waandishi wa habari 1,615 wameuawa tangu 1993, ambapo 34 wameuawa mwaka huu hadi sasa.

" Ripoti mbalimbali na taafiti pia zimethibitisha kuwa kumekuwa na vitisho dhidi ya na watu vikundi vidogo", alisema.

Uhalisia huu, aliongeza, unadhihirisha umuhimu wa haja ya kuwa makini katika kulinda wanahabari.

"Katika dunia ambapo taarifa ni nguvu", Jaji Aboud alisema "kuhakikisha usalama wa waandishi ni muhimu katika kulinda kanuni za demokrasi na haki za binadamu ".

Akisisitiza kuwa wanahabari ni wasimamizi wa ukweli, walinzi wa uwajibikaji, na kuzungumzia wasio na sauti, Jaji Aboud alisema kazi yao ni muhimu kwa kuwawajibisha walio madarakani, kuibua ukiukwaji wa haki na kuupatia umma taarifa za kuuwezesha kufanya maamuzi sahihi.

Akimkaribisha Jaji Aboud kufungua mkutano huo, Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga amesema ni ishara muhimu kwamba mkutano huo umefanyika katika Mahakama hiyo ya Afrika kwa sababu uhuru wa kujieleza ni haki ya msingi ya binadamu.

Alisema Mahakama ya Afrika ni nguzo ya haki za binadamu barani mwetu na uslama wa wanahabari ni suala muhimu kwa uhuru wa kujieleza.

"Kwamba Mahakama hiyo imekubali kufanyika kwa mazungumzo haya muhimu katika ukumbi wake ni uthibitisho tosha wa Imani ya Mahakama kuthamini kazi inayofanywa na waandishi wa habari. Pia ni kutambua kubadilishana huko mawazo kwa waandishi wa kanda ni muhimu kwa manufaa ya wanahabari, na pia demokrasia", Mukajanga aliongeza.

Mada mbalimbali kuhusu masuala ya usalama wa waandishi wa habari, ziliwasilishwa kwenye mkutano huo ukumbuni na kwa njia ya mtandao na wanahabari na wasemaji mbalimbali kutoka Tanzania Kenya, Uganda Zimbabwe, Sudan Kusini na Somalia.



Wawakilishi wa Umoja wa Kupata Taarifa (CoRI) wakiwa katika mafunzo mjini Moshi.

# CoRI waambiwa mafanikio ya sera yategemea ushiriki wa wanajamii

Na Saumu Mwalimu, Moshi

Mafanikio ya sera mbalimbali hutokea ikiwa wanajamii wanashiriki na kuguswa na utekelezaji wake.

Hili ni moja ya masuala yaliyojitokeza katika mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo wawakilishi wa taasisi zinazounda Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa (CoRI) yaliyofanyika Septemba 22-24, 2023 Weruweru mkoa wa Kilimanjaro.

Katika mafunzo hayo yaliyokuwa na malengo mbalimbali ikiwemo la kuongeza uwezo wa kufanya shughuli za uchechemuzi kwa wajumbe wa CoRI wakufunzi waliwaeleza washiriki kwamba moja ya mambo muhimu katika kutunga sera zinazotekelezeka na zenye kutatua changamoto halisi ni kuhakikisha wadau wote wanaoguswa na sera hizo wanashiriki kwa usawa.

Dk. Geofrey Chambua, mmoja wa wawezeshaji katika mafunzo hayo aliwaeleza washiriki kuwa hata wakati wa kuandaa miradi ni muhimu kuzingatia mnyororo wa watu watakaoathirika na miradi hiyo kwa kuhakikisha mchanganuo wa wanufaika wote unafanyika sawa.

“Kinyume na hapo kama ni mradi ama sera haitaleta usawa na utekelezaji wake unaweza usiwe na mafanikio kwa sababu kuna kundi litajisikia sio sehemu na hivyo kukwamisha mafanikio ya utekelezaji wake”, alisema Dk. Chambua.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, alisema kwamba MCT na washirika wake imekuwa ikifanya uchechemuzi wa sera na sheria kwa kipindi cha zaidi ya miongo miwili na kupata mafanikio mbalimbali.

“Moja ya mafanikio haya ni kuchukuliwa kwa maoni ya wadau katika Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003, lakini pia kuchukuliwa kwa mapandekezo ya wadau japo kwa uchache katika marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari 2016 yaliyoletwa mwaka huu wa 2023 kupitia Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali,” alisema Mukajanga.

Umuhimu wa kushirikishwa

Endelea Ukurasa wa 20

# Umuhimu wa elimu ya jinsia katika vyombo vya habari nchini

*Inatoka Ukurasa wa 17*

Zuhura Selemani kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alisema kuwa wakufunzi pia "tunalo jukumu kubwa la kuhakikisha tunawaongoza wanafunzi ili waweze kujua masuala ya haki na usawa wa jinsia, lakini pia sisi tuwe mfano wa kuigwa katika kuimarisha masuala hayo."

Aidha, Dk. Rehema Kilagwa kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Morogoro alisema kuwa waandishi wanafunzi nao wanapaswa kuwa imara ili kutekeleza kwa vitendo masuala ya haki na usawa katika kazi zao.

"Binafsi naona kuwa wakufunzi pia tuna dhima ya kuwaongoza wanafunzi wetu ili waweze kujua masuala ya haki na usawa wa jinsia", alisema.

Naye Athumani Gamba, mkufunzi toka Chuo cha Uandishi Habari cha Dar es Salaam (DSJ) alisema kuwa bado suala la jinsia lipo zaidi kinadharia hivyo juhudi zinahitajika katika kuimarisha suala hilo kwa vitendo.

Mafunzo hayo ya siku moja yalihusisha walimu zaidi ya 25 kutoka katika vyuo vya Kibaha Institute of Journalism Studies, Fanikiwa Journalism School (FJS), Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), Arusha East African Training Institute (AEATI), Dar es salaam School of Journalism (DSJ), Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU), Chuo Kikuu Cha Kiisilamu Morogoro (MUM), Dodoma Media College (DMC), na Rida Institute of Creative Knowledge and Innovative Skills.

Vyuo vingine ni pamoja na Chuo Kikuu Cha Tumaini kampasi ya Dar es Salaam (TUDARCO), Ujiji Broadcasting Academy, Chuo cha Taifa Zanzibar (SUZA), Mwenge Community College, Tabora East Polytechnic College, Huheso Institute of journalism and Community Development, Practical School of journalism, Habari Maalum College, Chuo Kikuu Iringa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC).

# Mafanikio ya sera yategemea ushiriki wa wanajamii

*Inatoka Ukurasa wa 19*

wadau ama jamii katika michakato ya utungwaji sera ama sheria ni muhimu kwa sababu husaidia jamii nzima kuwa katika ukurasa mmoja.

MCT na washirika wake wa CoRI wamekuwa wakishiriki katika michakato hii na kwa kupitia wao jamii imekua ikuhusishwa kwa namna tofauti tofauti kama kwa kupitia vipindi vya redio, makala za magazeti na machapisho mbalimbali, mafunzo na nyinginezo.

Wakizungumza wakati wa mafunzo hayo baadhi ya washiriki nao walisisitiza haja ya serikali kuhakikisha jamii nzima inashirikishwa katika michakato ya kutunga sera ama sheria kwa sababu jamii inao wataalamu ambao wataishauri serikali ama mamlaka inayotunga sera ama sheria hiyo.

"Mafunzo haya yametusaidia kugundua namna ambavyo jamii haihusishwi ipasavyo katika michakato ya utungwaji wa sera ama sheria na hii hupelekea wengi kutokuzijua na kufanya malengo ya sera hizo kutotimia ama kutotekelezwa ipasavyo," alisema Edwin Soko, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari wa Kupiga Vita Matumizi ya Dawa za Kulevya na Uhalifu Tanzania (OJADACT).

Mafunzo hayo ya siku tatu kwa wawakilishi wa CoRI yalilenga zaidi:

- Kuwaongezea zaidi ufahamu wa kufanya kazi zao katika umoja huo
- Kuboresha ujuzi wao wa uchechemuzi
- Kuongeza kujiamini na uwezo wa kuendesha uchechemuzi kwa hali ya juu
- Kuwawezesha kuandaa mkakati wa mawasiliano wa umoja huo
- Kuwawezesha wanachama kuandaa mpango wa utendaji kwa uchechemuzi bora.

Umoja huo ulioanzishwa 2006 kwa lengo la kuwa na sheria mpya ya haki ya kupata taarifa nchini na ile ya huduma za vyombo vya habari ulianzishwa na MCT, Taasisi ya Habari ya Kusini mwa Afrika - tawi la Tanzania (MISA-TAN) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA). Washiriuka hawa waliendesha harakati za kutungwa kwa sheria ya upatikanaji taarifa na sheria rafiki ya huduma ya vyombo vya habari.

Wanachama wa CoRI sasa wameongezeka na kuwa 16 ambapo wanachama waliongozeka ni Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Twaweza East Africa, JamiiForums, Policy Forum, Tanzania Citizen Information Bureau (TCIB), Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari (UTPC), Sikika, OJADACT, Tadio, Tanzania Online Media Network, na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Umoja wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS).



Waandishi Christopher Gamaina (kushoto) na Zephania Mandia (kulia) wakiwa pamoja na Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari ya Mwanza pose for a photo with the chairperson of (MPC) Edwin Soko (katikati).

# MCT yawapatia mafunzo mawakili zaidi

Na Mwandishi wa Barazani

Baraza la Habari Tanzania (MCT) linaendeleza jihihada za kuwafikia mawakili wengi zaidi ili kuwajengea uwezo wa kuelewa mazingira ya sekta ya habari lakini pia wawe na uwezo wa kusaidia ama kushauri waandishi pamoja na vyombo vya habari vinapokutana na kadhia mbalimbali zinazohitaji msaada wa kisheria.

Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga amesema hayo mjini Songea akifungua mafunzo yalilyoandaliwa na Baraza hilo kwa wanasheria. Mafunzo hayo ya siku tatu yalianza Septemba 13,2023.

Alisema licha ya hali ya uhuru wa habari kuonekana kuimarika nchini, zipo changamoto nyingi zisizoonekana moja kwa moja ambazo zimeendelea kukwaza haki hii muhimu ya kupata taarifa na kujieleza.

Mukajanga, amesema kuwa vyombo vya habari kama mmoja wakala muhimu katika kukuza na kutetea haki ya kujieleza bado vinaendelea kukutana na changamoto nyingi zinazokwamisha utendaji wao.

Alisema "pamoja na mabadiliko tunayoyaona ya sheria kadhaa, bado zipo changamoto za kisheria na zile zisizo za kisheria ambazo zinakwaza uhuru wa vyombo vya habari. Vyombo vya habari bado vinaendelea kupokea vitisho vya kiutawala , changamoto za kiuchumi na kibiashara na nyinginezo.

Katika wasilisho lake kuhusu sheria mahsusi za kusimamia uhuru wa kujieleza na jinsi zinavyohusu uhuru wa kiraia Wakili Fulgence Massawe amesema kua bado pamoja na marekebisho yanayoendelea kufanyika kwa ujumla wake sheria hizi zimesababisha uwepo mambo kadhaa ambayo yanafanya mazingira ya haki ya kujieleza na hata uhuru wa habari na vyombo vya habari kuwa magumu.

Alitaja baadhi ya mambo hayo ni pamoja na kuendelea kuwepo kwa watu kukamatwa kutoka na kutekeleza haki yao ya kujieleza, kupekua na kukamata mali, faini mbalimbali, kuharibiwa vifaa, kuchunguzwa ama kufuatiliwa mawasiliano binafsi.

Mengine ni watu kubambikiwa mashtaka/makosa ya jinai, kuzimwa kwa mawasiliano ya intanent, hofu ya kushtakiwa, kudhibitiwa katika maudhui katika vyombo vya habari ama mitandaoni.

"Lakini hivi mnajua wapo watu ambao imebidi waende kuishi uhamishoni baada ya vitisho walivyokua anavipokea kutokana na habari ama matamshi waliyokua wanayafanya," alisema Wakili Massawe wakati wa uwasilishaji wake.

Wakati huo huo imebainika kuwa wakati jitihada mbalimbali zikifanyika kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi katika sekta ya habari, changamoto hiyo pia imeonekana kuikabili sekta

Endelea Ukurasa wa 22

# MCT yawapatia mafunzo mawakili zaidi

*Inatoka Ukurasa wa 21*

ya sheria.

Katika mafunzo hayo kwa wanasheria , idadi ya wanawake walioshiriki katika mafunzo hayo ikiwa ndogo kulinganisha na wanaume.

Mafunzo hayo yaliyoshirikisha mawakili 20, ni mawakili wanawake sita tu walioshiriki ambapo wengine wakiacha kwa sababu mbalimbali.

Akifunga rasmi mafunzo hayo, Katibu Mtendaji wa MCT, Mukajanga, aliwahamasisha mawakili wanawake kuchangamkia fursa zilizopo kwenye uwanda wa haki za binadamu kwa kuwa kwa kiasi kikubwa mawakili waliopo katika kada hiyo ni wamaume.

"MCT inafanya kazi kwa karibu sana na mawakili mbalimbali kwa sababu shughuli zetu zinahitaji huduma hizo lakini mara nyingi tunakutana na mawakili wanaume, na kibaya zaidi ni wale wale wakati wote.

"Hivyo mafunzo haya yawe chachu kwenu kwa sababu huku tunapoelekea mawakili wenye uwezo wa kutetea masuala ya uminywaji wa haki za kujieleza na uhuru wa habari watahitajika zaidi," alisema Mukajanga.

Kwa upande wake Wakili Mwandamizi Mpale Mpoki alisema kuwa wao kama mabobezi katika kada hii ya haki za binadamu na mashauri ya kimkakati wapo tayari kutoa msaada na ushauri katika kuwajenga mawakili wachanga wanapokwama.

"Sio tu kwa wanawake hata kwa wanaume, kwa sababu ni ukweli usiopingika Tanzania hii mawakili wanaofanya kesi mkakati ni wachache, na wanawake ndio hamna kabisa….ni wa wachache na wa kutafuta, zipo fursa na tupo tayari kuwashika mkono," alisema Wakili Mpoki.

Hii ni awamu ya tatu kwa MCT kutoa mafunzo haya kwa mawakili yakiwa na lengo la kuwapatia uwezo na ufahamu wa hali ya uhuru wa kujieleza na wa vyombo vya habari, sheria za habari pamoja na mbinu za kushughulikia mashauri ya kimkakati ya masuala ya habari na uhuru wa kujieleza.

Mawakili waliohudhuria mafunzo hayo wametoka mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Arusha, Dodoma na Ruvuma.

Mafunzo mengine kama haya yalifanyika mwaka 2021 Jijini Tanga na Visiwani Zanzibar mwaka 2022 chini ya mradi ulifadhiliwa na International Media Support (IMS). Jumla ya mawakili 55 wamepatiwa mafunzo haya.



*Mawakili waliopatiwa mafunzo na Baraza la Habari Tanzania mjini Songea wakiwa pamoja na Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga walioketi mbele katikati ambapo upande wa kushoto na kulia ni wawezeshaji wa mafunzo hayo mawaikili Fulgence Massawe na Mpale Mpoki.*

# Nimekamilisha, asema Mukajanga


*Inatoka Ukurasa wa 8*

hupenda kunikumbusha kuwa tulikutana na Rais Mohammed Shein Ikulu tarehe 12 Machi 2012 na Rais Husein Mwinyi tarehe 22 Desemba 2022.

Kwa pamoja, tumewasaidia waandishi wanawake kupata stadi mbalimbali ikiwa ni pamoja na menejimenti ya vyombo vya habari, lakini pia tumeandika kitabu cha kufundishia masula ya jinsia kwa waandishi. Tumeandaa Sera ya Jinsia katika Vyombo vya Habari, na tunawalea waandishi kupitia mentoring program ya mradi wa Wanawake katika Vyombo vya Habari.

Kwa pamoja, tumeshinda changamoto za kifedha, na kuweza kudumu kwa muda wote huu. Tumepata mafanikio mengi; siwezi kuyataja yote hapa. Leo nakuageni, nikijivuna kwamba tumelijenga Baraza pamoja, na kulifanya taasisi inayoheshimika na inayotuheshimisha, na sisi kuwa na fahari kuifanyia kazi.

Nakushukuruni sana wafanyakazi wenzangu. Mmekuwa timu isiyojua kushindwa, timu ambayo neno 'kukata tamaa' halikuwa katika msamiati wenu. Asanteni sana.




*Baadhi ya machapisho ya Baraza la Habrai Tanzania (MCT)*

Na kwa wanachama wa MCT, nawasihi muendelee kudumisha mshikamano. Muendelee kuliunga mkono Baraza lenu. Naamini pia kwamba leo mtatuchagulia Bodi ya watu wanaoamini katika uhuru wa habari, kusimamia umahiri katika taaluma, na muhimu kabisa, waumini wa umuhimu wa sekta hii kujisimamia, yaani self-regulation. Kwa maana huko tuendako, mfumo huu utakumbana na changamoto mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waheshimiwa wajumbe, Mungu atubariki sana, Mungu ibariki Media Council of Tanzania.

***Asanteni kwa kunisikiliza.***

# Tido atunukiwa LAJA

*Inatoka Ukurasa wa 16*

Kwa sababu ya gharama kubwa ya kazi hii, serikali ikawaruhusu watafute kampuni ya nje kwa ajili ya ubia. Baada ya mchakato wa manunuzi, bodi ya TBC ikaichagua kampuni ya Kichina ya Startimes.

Licha ya kufanikisha maboresho TBC, ghafla 14 Desemba 2010, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari huyo alimwita ofisini kwake na kumkabidhi barua, akimwambia anatakiwa kukabidhi ofisi na kuondoka TBC siku inayofuata.

Machozi yalimlengalenga lakini hakuwa na la kufanya, akajua licha ya kwamba mkataba wake ulikuwa kweli umefika mwisho, lakini kwa notisi ile ya chini ya saa 24, ilikuwa ni sawa na kwamba amefukuzwa kazi.

Mwezi mmoja baada ya kuachishwa kazi TBC, Tido, alipokea simu kutoka kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Nation Media Group ya Kenya ambao pia ndiyo wamiliki wa kampuni ya magazeti ya Mwananchi, MCL, akimtaka aende kuingoza kampuni hiyo ya Mwananchi, hata kama ni kwa muda mfupi.

Alisita kwa kuwa hakuwa na uzoefu hata kidogo wa biashara ngumu ya uchapishaji, usambazaji na uuzaji wa magazeti. Lakini baada ya kupata ushauri kutoka kwa aliyekuwa mwenyekiti wa bodi ya MCL, Zuhura Muro, na wana bodi wengine, akakubali.

Mkataba wake na Mwananchi ulipomalizika tu mwaka 2014 akajiunga na Azam Media Limited.

Miaka minane baadae akiwa, Azam Media, akafunguliwa kesi akishtakiwa kwa matumizi mabaya ya madaraka na kuisababishia hasara serikali wakati wa kipindi chake cha uongozi TBC, hususan kuhusu ule mradi wa usambazaji wa mfumo wa kidigiti.

TIDO aliposomewa mashtaka hayo mahakamani Kisutu alijisemea kimoyomoyo kwamba aliyeyaandika ama hakuyadhamiria kwake, au hakumjua vizuri. Anakiri kwamba mwekezaji mmoja aliyehusishwa na kesi ile alitaka kumpa dola milioni moja ili apate upendeleo; akakataa na kumwambia heshima yake na ya Tanzania ni ya thamani kubwa kuliko hizo fedha. Mtu huyo akakasirika sana.

Hata hivyo, hatimae mahakama ilikuta Tido hana hatia na kumwachia huru. Nguli wengine wa habari waliotunukiwa Tuzo ya LAJA ni Fili Karashani (marehemu), Hamza Kassongo, Mariam Hamdani, Rose Haji, Jenerali Ulimwengu na Ndimara Tegambwage.




*Afisa Programu wa MCT, Saumu Mwalimu, akimkabidhi Sera ya Jinsia Katika Vyombo vya Habari kwa Mhariri Mkuu wa Redio Jogoo FM, Aden Mbele na Mhariri Mkuu Msaidizi wa Key FM Stella Hamisi wakati MCT ilitembelea vyombo hivyo Mjini Songea Mkoani Ruvuma.*

# Waandishi wahimizwa kutafuta maarifa

**Na Mwandishi wa Barazani**

"Wanasema kujifunza hakuna mwisho na maarifa hutafutwa".

Hayo ni maneno ya Stella Hamisi Mkuu Mhariri Msaidizi wa Redio Key FM ya Mjini Songea wakati maafisa wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) walipowatembelea wadau wa habari katika Mjini Songea Mkoani Ruvuma.

MCT ilikuwa Mjini Songea kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya siku tatu kwa mawakili yaliyofanyika Septemba 12 hadi Septemba 14, 2023.

Ikiwa Songea, MCT iliwatembelea wa habari wake ambao ni redio Jogoo FM pamoja na Key FM ambapo mambo kadhaa ya kitaaluma yalijadiliwa katika ziara hizo ikiwemo kwa waandishi wa pembezoni kutafuta fursa za kujiendeleza kupitia majukwaa mbalimbali.

Stella ambaye alianza kwa kuipongeza MCT kwa program mbalimbali za mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma ambayo yeye amekuwa ni mmoja wa wanufaika alisema pamoja na kwamba waandishi wengi wa pembezoni hususani kutoka vyombo vya habari vidogo kama redio za mikoa wamekuwa wakikosa fursa za mafunzo ni muhimu wachukue jitihada ya kuzitafuta fursa kwa sababu zipo, na zipo taasisi nyingi ikiwemo MCT ambayo zinatoa mafunzo fursa hizo.

"Tutengeneze 'network' utaotuwezesha kupata taarifa mbalimbali juu ya fursa nyingi zilizopo huko nje, zipo nyakati tunalalamika kwamba hatupati nafasi ya kujiendeleza lakini tujiulize sisi wenyewe tumechukua hatua gani kujua nani anatoa fursa za kujiendeleza na kuomba", alisema Stella.

Katika ziara hiyo kwa wadau wa habari MCT ilipata nafasi ya kuzungumzia pia Sera ya Jinsia Katika Vyombo vya Habari na umuhimu wake katika kushawishi uwepo wa usawa wa kijinsia katika ngazi mbalimbali za vyumba vya habari lakini pia kupitia maudhui yanayotolewa na vyombo vya habari.

Akizungumza katika ziara hizo Afisa Programu wa MCT, Paul Mallimbo alieleza umuhimu wa vyombo vya habari kuwa na sera mbalimbali ikiwemo hii ya Jinsia Katika Vyombo vya Habari kuwa inasaidia kuweka mwongozo na msingi ambao chombo cha habari kitatumia katika utendaji kazi wake. "

Sera hii inaeleza hata jinsi unapotaka kuajiri mfanyakazi upitie hatua zipi katika suala zima la kuzingatia usawa unakuepo, au unapomtuma mwandishi kwenda kutafuta habari afanye nini ili habari yako iwe imezingatia jinsia," alisema Mallimbo.

Kwa upande wake Mhariri Mkuu wa Redio Jogoo FM ya Mjini Songea, Aden Mbele nayee alisisitiza umuhimu wa vyombo vya habari kuzingatia sera hizi huku akiahidi kuwa chombo chake kitaizingatia sera ya MCT na kuona namna bora ya kutekeleza.